

HALMASHAURI YA WILAYA YA MKINGA



Kumb Na: HW/MKG/S.85/20/61

11.08.2020.

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mkinga amepata kibali cha ajira mbadala kutoka kwa Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora,kupitia barua yenyewe Kumb Na 170/369/01" A"/72 ya tarehe 01 Julai ,2020,hivyo anapenda kuwatangazia Watanzania wote wenye sifa kuwasilisha maombi ya kujaza nafasi za kazi kama ifuatavyo:-.

1.0 Mtendaji wa Kijiji III – Nafasi 1

Ngazi ya Mshahara: TGS B

1.1 Kazi na Majukumu ya Mtendaji wa Kijiji III.:

- i. Afisa Masuuli na Mtendaji Mkuu wa Serikali ya Kijiji,
- ii. Kusimamia Ulinzi na Usalama wa raia na mali zao, kuwa Mlinzi wa Amani na Msimamizi wa Utawala Bora katika Kijiji.
- iii. Kuratibu na kusimamia upangaji na utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo ya Kijiji;
- iv. Katibu wa Mikutano na Kamati zote za Halmashauri ya Kijiji;
- v. Kutasfiri na Kusimamia Sera, Sheria na Taratibu:
- vi. Kuhamasisha wananchi katika kuandaa na kutekeleza mikakati ya kuondoa njaa, umasikini na kuongeza uzalishaji mali;
- vii. Kiongozi wa Wakuu wa Vitengo vya Kitaalam katika Kijiji;
- viii. Kusimamia, kukusanya na kuhifadhi kumbukumbu zote na Nyaraka za Kijiji;
- ix. Mwenyekiti wa Kikao cha Wataalamu walipo katika Kijiji;
- x. Kupokea, kusimamia utungaji wa Sheria Ndogo za Kijiji; na
- xi. Atawajibika kwa Mtendaji wa Kata.

1.3 Sifa za Mwombaji

Awe mhitimu wa Kidato cha Nne au cha Sita mwenye Cheti cha fani ya Utawala,Sheria,Rasilimali watu,Maendeleo ya jamii au usimamizi wa fedha kutoka chuo kinachotambuliwa na Serikali

2.0 Mhudumu wa Jikoni - Nafasi -1

2.1 Ngazi ya Mshahara: TGOS A

2.2 Kazi na Majukumu ya Mhudumu wa Jikoni

- i. Kusafisha Vyombo vya Kupikia.
- ii. Kusafisha Vyombo vya Kulia chakula.

- iii. Kusafisha Meza itumikayo kwa kulia chakula.
- iv. Kuwatayarishia Wapishi/waandazi Vifaa vya Mpishi na Mezani na
- v. Kusafisha maeneo ya kulia chakula na kupikia.

3.3 **Sifa za Mwombaji:**

Awe muhitimu wa Kidato cha Nne mwenye uzoefu wa kazi kwa muda usiopungua miaka mitatu.

AJIRA YA MKATABA WA MWAKA MMOJA

3.0 Afisa Msaidizi wa Hesabu II - Nafasi -1

3.1 Ngazi ya Mshahara: TGS B

3.2 Majukumu ya kazi:-

- i. Kuandika na kutunza “regester” zinazohusu shughuli za Uhasibu.
- ii. Kutunza majalada yenyekumbukumbu za Hesabu,
- iii. Kuandika hati za malipo na hati za mapokezi ya fedha,
- iv. Kupeleka barua/nyaraka za Uhasibu Benki.
- v. Kufanya usuluhishi wa masurufu na hesabu za Benki na
- vi. Kufanya kazi nyingine za fani yake atakazopangiwa na Mkuu wake wa kazi.

3.3 **Sifa za Mwombaji**

Awe na cheti cha Astashahada ya uhasibu kutoka chuo kinachotambulika na Serikali au cheti cha ATEC II kinachotolewa na NBAA au sifa nyingine zinazolingana .

MAELEKEZO YA JUMLA

1. Mwombaji awe Raia wa Tanzania na awe tayari kufanya kazi kokote atakapo pangiwa ndani ya Halmashauri ya Wilaya ya Mkinga.
2. Mwombaji awe na umri kati ya miaka 18-45.
3. Mwombaji awe hajawahi kupatikana na kosa la jinai au kufungwa jela.
4. Maombi yote yaambatane na Wasifu wa mwombaji (CV).
5. Maombi ya ambatanishwe na nakala za vyeti vya Elimu, vyeti vya taaluma, cheti cha kuzaliwa na picha mbili za (passport size) zilizoandikwa jina la Mwombaji nyuma.
6. Testimonials “Provisional Results”, “Results Slips”, kiapo cha kuthibitisha umri wa kuzaliwa **HAVITAKUBALIWA**.
7. Barua ya maombi iandikwe kwa mkono na kutumwa kwa njia ya Posta.
8. Waombaji ambao walisoma nje ya nchi vyeti vyao vya Taaluma vifanyiwe ulinganishi na TCU na NECTA na majibu ya ulinganisho yaambatanishwe kwenye barua ya kazi.
9. Waombaji waliowahi kuacha kazi, kuachishwa au kufukuzwa kazi hawaruhusiwi kuomba isipokuwa kama ana kibali cha Katibu Mkuu Kiongozi cha kuajiriwa tena.
10. Mwombaji ambaye ni Mwajiriwa wa Serikali anatakiwa kuitishia barua yake kwa Mwajiri wake wa sasa.

11. Mwisho wa kupokea maombi ya kazi ni tarehe **31/08/2020 saa 9:30 Alasiri.**
12. Tangazo hili linapatikana pia kupitia tovuti ya Halmashauri: www.mkinga.go.tz

Maombi yote yatumwe kwa njia ya **Posta** kwa: -

MKURUGENZI MTENDAJI WILAYA,
HALMASHAURI YA WILAYA YA MIKINGA,
S.L.P 6005,
TANGA.



Rashid K. Gembe

**MKURUGENZI MTENDAJI WILAYA
MKINGA**

MKURUGENZI MTENDAJI (W)
MKINGA